UFUGABI BORA WA NGURUWE

UFUGAJI BORA WA NGURUWE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO NA USHIRIKA

© Wizara Ya Kilimo Na Ushirika
Dar Es Salaam - Tanzania

Toleo la Kwanza 1986
Toleo laPili 1998

ISBN 9987 647 01 4

Kimetayarishwa na Wizara ya Kilimo na Ushirika, Kitengo cha Elimu kwa Wakulima, Chini ya Mpango wa Taifa wa Huduma za Ushauri (NAEP II)

Kimehaririwa na:-

Hamis L. Nyangi - Elimu kwa Wakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika, Dar es Salaam.

Happiness Mlaki - Elimu kwa Wakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika, Dar es Salaam.

Dorcas Shempemba - Elimu kwa Wakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika, Dar es Salaam.

Caroline Swai - Elimu kwa Wakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika, Dar es Salaam.

M.K. Nyanda - Elimu kwa Wakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika, Dar es Salaam.

Luitgard Lupenza - Elimu kwa Wakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika, Dar es Salaam.

Asmin Munisi - Elimu kwaWakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika, Dar es Salaam.

Elias Sabuni - Elimu kwa Wakulima, Wizara ya Kilimo na Ushirika. Dar es Salaam.

Dr. G. Laswai - Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine Morogoro.

O.G. Mmari - Jeshi la Kujenga Taifa Makao Makuu, Dar es Salaam.

Utangulizi

Nchini Tanzania ufugaji wa nguruwe unazidi kuongezeka siku hadi siku. Hii ni kwa sababu, nguruwe ni moja kati ya mifugo inayompatia kipato mfugaji kwa haraka, kwani huzaa mara mbili kwa mwaka na kila mzao anaweza kuzaa watoto 12. Licha ya kuzaa mara mbili, mnyama huyu hukua na kuongezeka uzito baraka. Kwa siku huweza kuongezeka uzito wa gramu 500 hadi 700 na hivyo kufikia uzito wa kuchinjwa (kilo 60 hadi 90) mapema, kati ya miezi sita hadi nane kama atatunzwa vizuri.

Vile vile gharama za kufuga nguruwe ni ndogo ukilinganisha na gharama za kuwafuga wanyama wa aina nyingine kwani nguruwe anaweza kula mabaki ya vyakula kutoka mashuleni, mahotelini, majumbani na mahospitalini. Halikadhalika huweza kula mboga na matunda ambayo yameharibikabustanini kamavilenyanya, mapapai, kabichi na maboga.

Nguruwe hufugwa kwa ajili ya nyama, mafuta na mbolea. Hatahivyo wafugaji wengi hufuga ngumwe bila kuzingatia kanuni za ufugaji bora ambazo ni pamoja na uchaguzi wa njia za ufugaji na utunzaji bora wa ngumwe, dume, jike na watoto. Ili ngumwe aweze kutoa mazao mengi na bora anatakiwa kulishwa chakula bora na kilichochanganywa vizuri, kufugwa kwenye nyumba bora, pia kumkinga na kumtibu dhidi ya magonjwa na matatizo mbali mbali. Vile vile, ubora wa mazao ya ngumwe unategemea kwa kiasi kikubwa utayarishaji wa mazao kabla ya kuuza. Ubora wa nyama unaweza kuharibika endapo taratibu za utayarishaji na hifadhi bora ya mazao hazitafuatwa. Aidha mfugaji anatakiwa kuzingatia uwekaji wa kumbukumbu.

Kitabu hiki kimetayarishwa ili kumsaidia mkulima kufuga nguruwe kitaalam. Endapo maelezo yaliyomo katika kitabu hiki yatazingatiwa wafugaji watapata mazao mengi nabora nahivyo kuwaongezeapato na kuweza kuboresha afya za familia zao na hatimaye Taifa zima.

SURA YA KWANZA

NJIA NA AINA ZA UFUGAJI

Mkulima anayehitaji kufuga nguruwe anapaswa kufahamu njia na aina za ufugaji. Njia na aina hizo hutegemea mahali, eneo na uwezo wa mfugaji.

Njia za Ufugaji

Kuna njia kuu tatu za kufuga nguruwe nazo ni:

õ **Ufugaji huria.**

- Nguruwe huachwa wajitafutie chakula wenyewe.
- Hupewa hifadhi wakati wa usiku.

Faida:

- Hainagharamakubwakwamfugaji.
- Huweza kujipatia madini hasa ya chuma kwa urahisi.
- Hurutubishaudongokwakinyesinamkojowake.

Hasara:

- Ni rahisi kuibiwa au kuliwa na wanyama wakali.
- Huharibu mazao shambani na mazingira.
- Hupata magonjwa na minyoo kwa urahisi na huweza kusambaza kwabinadamu.
- Huzaliana bila mpango.
- Huhitaji eneo kubwa.

õ **Ufugaji wa Ndani na Nje.**

- Ngumwe hufungiwa ndani ya uzio ambapo kuna banda maalumu.
Hupewa chakula na maji na ana uhum wa kuingia na kutoka ndani ya banda.

Faida:

- Si rahisi kuambukizwa magonjwa kutoka nje ya uzio.
- Njia hii inapunguza upotevu, wizi na kushambuliwa na wanyamawakali.
- Mazao yake ni mengi kuliko ya njia ya huria.
- Ni rahisi kuwahudumia kwa chakula na magonjwa.
- Ukusanyaji wa mbolea ni rahisi.

Hasara:-

- Gharama kubwa kuliko zaufugaji huria.
- Ni rahisi kuambukizana magonjwa na minyoo.

- Huhitaji eneo kubwa.
- Mfugaji analazimika kumpatia chakula na maji.

õ **Ufugaji wa Ndani**

Nguruwe hujengewa banda ambalo hugawanywa kufuatana na makundi; kwa mfano ngumwe dume, jike na vitoto. Katika ufugaji huu nguruwe hupewa chakula na maji ndani ya banda.

Faida:

- Ni rahisi kuwahudumia kwa chakula, kinga na tiba
- Ni rahisi kuthibiti magonjwa, minyoo na wadudu wengine.
- Ni rahisi kusimamia uzalishaji wa aina unayoitaka kwa wakati unaotakiwa.
- Hutoa mazao mapema, mengi na bora.
- Hawadhuriki na wanyama wakali na si rahisi kuibiwa
- Huhitaji eneo dogo.

Hasara:

- Huhitaji mtaji mkubwa
- Huhitaji uangalizi wa karibu na wa kitaalam
- Huweza kuambukizana magonjwa.

Aina za Ufugaji wa Nguruwe

Kuna aina nne za ufugaji ambazo mfugaji anaweza kuchagua ili kuongeza mapato yake.

(i) Nguruwe waliotenganishwa na mama yao baada ya kutimiza miezi miwili.

Mfugaji anahitaji kuwa na majike kwa ajili ya uzalishaji.

(ii) Kununua ngumwe waliotenganishwa na mama yao na kuwatunza kwa ajili ya nyama na mafuta.

(iii) Kukuzajike na dume na kutunza watoto mpaka wanapofikia umri wa kuuzwa kwa ajili ya nyama.

(iv) Ufugaji kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora. Njiahhni ngumu ina gharama kubwa, na inahitaji utaalam zaidi.

SURA YA IPLI

UCHAGUZI WA NGURUWE BORA

Ili kuweza kupata mazao mengi na bora ni muhimu kwa mkulima kuchagua nguruwe wenye sifa zifuatazo,

Sifa za Nguruwe Bora

Dume:

- Asichaguliwe kutoka kwenye ukoo wenye historia ya magonjwa au kilema cha kurithi.

- Awe na miguu imara, mchangamfu na mwenye afya bora.

- Awe na umbile zuri na misuli imara itakayomuwezesha kupanda bila matatizo.

- Awe mwenye kende zilizokamilika.

- Awe anayekua haraka na mwenye uwezo mkubwa wa kubadili chakula kwa matumizi ya mwili kuwa nyama.

Jike:

- Awe na umbile la kumuwezesha kubeba mimba na kuzaa kwa urahisi.
- Awe na chuchu zisizopungua 12 na ziwe zimejipanga vizuri.

Aina Za Nguruwe

Kuna aina nyingi za nguruwe wafugwao, zifuatazo ni baadhi ya aina zinazofugwa hapa nchini.

õ Nguruwe Mkubwa Mweupe

- Ni mweupe, masikio yake yamesimama na paji la uso limeingia ndani kama bakuli.
- Si rahisi kushambuliwa na magonjwa.
- Wenye umri mdogo, nyama yake haina mafuta mengi.
- Hukua na kuongezeka uzito kwa haraka sana.
- Jike hutoa maziwa mengi
- Dume hutumika kwa ajili ya kuboresha aina nyingine za nguruwe.



Nguruwe Mkubwa Mweupe

õ **Nguruwe Mrefu Mweupe (Landrace)**

- Huyu ni mrefu mweupe na mwembamba kuliko yule mkubwa mweupe.

- Masikio yake yameinama kwa mbele.

- Haongezeki uzito upesi na hutoa nyama isiyo na mafuta mengi.

- Aina hii ikipandishwa na aina ya kwanza huzaa nguruwe anayetoa mnofu mzuri zaidi usiokuwa na mafuta mengi.



Nguruwe Mrefu Mweupe [Landrace]

õ **Nguruwe Mfupi Mweusi, mwenye mstari mweupe kuzunguka mwili kwenye miguu ya mbele (Wessex Saddleback)**

- Ni mfupi, mweusi na ana mstari mweupe kuzunguka mwili kwenye miguu ya mbele.
- Masikio yameinama.
- Mgongo umepinda kidogo mfano wa upinde.
- Hutoa mafuta mengi sana.
- Hutoa maziwa mengi, huzaa watoto wengi na kuwatunza vizuri.



Nguruwe mfupi Mweusi mwenye mstari mweupe kuzunguka mwili kwenye miguu ya mbele [Wessex Saddleback]

õ **Nguruwe Chotara:**

- Ni uzao unaotokana na kupandisha nguruwe wa aina mbili tofauti.
- Nguruwe wa kienyeji akipandishwa na wa kisasa (kigeni).
- Anastahimili magonjwa, anakua haraka na nyama yake huwa haina mafuta mengi.
- Anastahimili mazingira magumu kuliko wa kisasa.

õ **Nguruwe wa Kienyeji**

- Huwa ni wadogo kwa umbo.
- Wanakua taratibu hata kama wanapatiwa chakula bora.
- Hawana rangi maalum.
- Hustahimili mazingira magumu.
- Nyamayakehainamafutamengi.
- Wana uwezo wa kujitafutia chakula.



Nguruwe wa Kienyeji

SURA YA TATU

UTUNZAJI WA NGURUWE

Utunzaji wa nguruwe mara nyingi hutegemea aina ya nguruwe, njia na aina ya ufugaji. Kwa mfano nguruwe jike anayefugwa kwa ajili ya kuzaa anahitaji kutunzwa tofauti na wale wanaonenepeshwa kwa ajili ya nyama. Kadhalika nguruwe wanaweza kufugwa ndani ya banda au nje, kutegemea na ukubwa wa shamba, fedha zilizopo kwa shughuli za ufugaji na aina ya nguruwe.

Utunzaji wa Nguruwe Dume

Achaguliwe dume mwenye sifa bora ikiwa ni pamoja na kutokuwa na kilema au ugonjwa wowote. Dume aliyechaguliwa, atenganishwe na majike ili kuepusha kupanda wakati usiotakiwa. Inabidi nguruwe huyu asinenepeshwe, kwa hiyo alishwe chakula bora kiasi cha kilo mbili hadi tatu kwa siku. Vile vile apewe maji kila siku.

Kama anapanda chini ya mara tatu kwa wiki, alishwe kilo mbili na nusu na kama anapanda zaidi ya mara tatu, alishwe kilo tatu kwa siku. Ikiwa dume ni dhaifu, aongezewe nusu kilo ya chakula na kama amenenepa sana apunguziwe nusu kilo ya chakula kwa siku. Ni muhimu awe na eneo la mita mraba 9.3 ilikuwezakupata mazoezi ya mwili. Ikiwa sehemu ya kupanda imetenganishwa eneo livve la mita mraba saba.

Nguruwe dume anaweza kutumika kwa kupandajike akiwa na umri wa miezi minane hadi tisa. Kwa umri huu anaruhusiwa kupanda jikemojakwajuma. Afikiapo miezi 10 anaruhusiwa kupanda majike mawili hadi matatu kwajuma. Akiwana umri wa mwaka mmoja au zaidi ana uwezo wa kupandajike mmoja kila siku kwa majuma mawili hadi malatu, kisha apumzike kwa muda wa majuma mawili. Dume wakubwa wasitumike kupandajike wadogo kwani vvanaweza kuleta madhara kama vile kuwavunja mgongo.

Ni vizuri nguruwe dume mmoja apandejike 15 hadi 20 kwa mwaka. Dume akizeeka au kuwa na ubovu wa miguu, achinjwe mara moja. Ni muhimu dume aogeshwe kwa sabuni na dawa zinazoweza kuua wadudu na vijidudu vinavyoweza kusababisha magonjwa. Banda na vifaa vinavyotumika visafishwe kila siku.

Utunzaji Wa Nguruwe Jike

Ili mfugaji aweze kupata mazao mengi na bora hana budi kuchagua ngumwejike mwenye sifa zinazotakiwa. Nguruwe huyu ni vizuri awe amezaliwa na mama anayezaa watoto wengi, mwenye kutoa maziwa mengi na mtunzaji mzuri wa watoto. Tabia hizi zinarithiwa hata navizazi vingine vijavyo. Vile vile awe na afyanzuri na chuchu nyingi zisizopungua 12.

Nguruwe jike anaweza kuzaa akiwa na umri wa miezi mitano hadi sita. Ili kumzuia asibebe mimba mapema, ni vizuri atenganishwe na dume afikiapo umri huo.

Afikiapo miezi nane hadi tisa au akiwa na uzito wa kilo 130 ahaweza kupandishwa. Kabla ya kupandishwa nguruwejike apewe kilo 2.5 hadi tatu za chakula kwa siku. Nguruwe asipelekwe kwa dume mpaka atakapoonyesha dalili zajoto.

õ **Dalili za Joto:**

- Kutopenda kula chakula.
- Kupiga kelele ovyo.
- Kuhangaika kila mara.
- Hupenda kupanda au kupandwa na nguruwe wenzake.
- Sehemu ya uke huvimba na huwa nyekundu.
- Hukojoa mara kwa mara na hutoa ute mweupe usiokatika.
- Hutulia anapokandamizwa mgongoni.

Dalili hizi sio lazima zionekane zote kwa wakati mmoja hivyo ni jambo la muhimu kuwa mwangalifu.

Ili dalili hizi ziweze kuonekana vizuri, chumba cha majike yanayotarajiwa kupandwa kinatakiwa kiwe karibu na cha dume. Joto hudumu kwa muda wa siku mbili hadi tatu. Ngumwe Jike apandishwe mara anapokua kwenye joto na kumdia tena katika muda wa masaa 12. Baada ya kupandishwa huchukua miezi mitatu, wiki tatu, siku tatu (siku 114 hadi 119) hadi kuzaa. Ngumwejike wawekwe kwenye banda lenye nafasi, hewa ya kutosha na uzio wa kutosha kwa ajili ya mazoezi.

õ **Kutunza Nguruwe Mwenye Mimba.**

Nguruwe wenye mimba wanahitaji mazoezi zaidi ili kuimarisha miguu na misuli yao, hivyo banda liwe na uzio wanapoweza kutoka na kucheza. Sehemu ya uzio isiwe na unyevu ili wasipate magonjwa, ikiwezekana kuwe na kivuli cha kuwakingajua.

Mandalizi ya Chumba cha Kuzalia

Wiki mbili hadi tatu kabla ya nguruwe kuzaa andaa chumba cha kuzalia. Chumba hiki kiwekwe boriti au reli kuzunguka ili kutenga sehemu ambayo itahifadhi watoto wasilaliwe au kukanyagwa na mama yao (angalia mchoro sura ya tano).

Vile vile chumba hiki kiwe na sehemu ya kuweka chombo cha kuongezeajoto, chakula na maji kwa ajili ya watoto.

Maandalizi Kabla ya Kuzaa

Wiki moja kabla ya kuzaa ngumwe aogeshwe vizuri kwa maji safi na sabuni. Baada ya kuogeshwa anyunyiziwe dawa ili kuzuia wadudu wa ngozi na apewe dawa ya minyoo. Kisha ahamishiwe kwenye chumba cha kuzalia.

Nguruwe mwenye mimba anahitaji kupewa chakula kinacholeta nguvu na kujenga mwili. Katika mwezi wa kwanza apewe kilo 2 hadi 2.5 kwa nguruwe mwenye afya nzuri, akiwa dhaifu apewe kilo 3 kwa majuma matatu.

Mwezi wa pili mpaka siku ya tatu kabla ya kuzaa alishwe kilo 3.5 za chakula. Siku ya tatu kabla ya kuzaa, chakula kipunguzwe hadi kufikia kilo 2 kwa siku. Siku ya kuzaa asipewe chakula bali apewe maji tu.

Dalili za Kuzaa

Kuna dalili ambazo ngumwe huonyesha kabla hajazaa. Dalili hizi zionekanapo kuna umuhimu wa kuwepo mwangalizl ili aweze kutoa msaada kama itabidi, hasa kwa nguruwe anayezaa kwa mara ya kwanza.

- Kiwele na chuchu huwa kubwa kwa kujaa maziwa.
- Njia ya uke huvimba na kuwa nyekundu na mara nyingine hutoa maji mazito.
- Nguruwe huhangaika na hupumua kwa nguvu,
- Maziwa yanaweza kutoka yenyewe kwenye chuchu
- Hukojoa mara kwa mara
- Hukusanya majani na kuandaa mahali pa kuzalia
- Tumbo linapwelea na baadhi hupbteza hamu ya kula.

Utunzaji Baada ya Kuzaa

Mwangalizi ahakikishe kuwa watoto wananyonya na kuwaweka mahali penyejoto la kutosha. Vitovu vikatwe na kuachwa sentimita tano kwa kutumia vifaa visafi, na kisha paka dawa yajoto (lodine tincture) kuzuia magonjwa.

Kondo la nyuma likidondoka litupwe na hakikisha limetoka lote kwa kuhesabu vipande kulingana na idadi yawatoto. Endapo idadi haikulingana, unashauriwa kumwona mtaalam wa mifugo aliyekaribu nawe.

Baada ya nguruwe kuzaa apewe ongezeko la kilo moja ya chakula kila siku hadi siku ya nne. Kuanzia siku ya tano hadi ya nane apewe hadi kilo nne. Baada ya hapo apewe kilo tatu na moja ya tatu ya kilo kwa kila mtoto. Kwa mfano nguruwe mwenye watoto 12 apewe chakula kiasi cha kilo saba; (kilo 3 + 1/3 x 12 = 7).

Vile vile apewe maji ya kutosha wakati wote. Kumbuka nguruwe akilishwa chakula kingi, atanenepa sana na hatapata mimba kwa urahisi na akibahatika kupata huweza kuharibika. Akilishwa chakula kidogo hudhoofika, huzaa watoto dhaifu na hutoa maziwa kidogo. Siku ya kuwatenganisha watoto na mama yao

punguza chakula mpaka kilo mbili kwa siku. Siku inayofuata ongeza hadi kufikia kilo 2.5 mpaka tatu kutegemea na afya ya mama.

Nguruwehurudi kwenyejoto baada ya siku tano hadi kumi baada ya kuachisha kunyonyesha.

Utunzaji wa Watoto

• Ulishaji wa Maziwa ya Kwanza

Mara tu baada ya kuzaliwa hakikisha kuwa vitoto vinanyonya maziwa ya kwanza. Maziwa haya ni muhimu kwani yana viinilishe vya kujenga mwili, kuleta nguvu na kuongeza kinga dhidi ya maradhi.

Kama mama amekufa mara tu baada ya kuzaa na hakuna nguruwe mwingine anayeweza kuwanyonyesha, wapewe maziwa ya kwanza ya ng'ombe. Endapo yatakosekana wapewe mchanganyiko maalum wa maziwa ya ng'ombe.

• Joto

Watoto wa nguruwe huzaliwa bila manyoya na huwa hawana mafuta mengi ya kutosha kuwapatiajoto mwilini. Kwenye sehemu za baridi ni jambo la muhimu kuwapatiajoto kwa kutumia umeme au chemli.

• Kuzuia Upungufu wa Damu

Nguruwe huzaliwa wakiwa na upungufu wa madini ya chuma. Halikadhalika maziwa ya mama yao huwa na upungufu wa madini hayo, hivyo wasipopatiwa madini hayo hupata upungufu wa damu, hudhoofika na hatimaye hufa.

Ili kuepuka tatizo hili watoto wapatiwe madini ya chuma kwa kutumia mojawapo ya njia zifuatazo:

- Kudunga sindano ya madini hayo kwenye misuli siku mbili hadi tatu baada ya kuzaliwa.

- Kupaka madini ya chuma kwenye chuchu za mama.

Changanya kilo moja ya madini ya chuma kwenye lita mbili za majimoto.

- Kuwanywesha maji yenye madini ya chuma mililita moja na nusu kwa mwezi mmoja.

- Kuwapa udongo msafi.

- Watoto wanaotunzwa kwenye sakafu ya saruji au mbao waruhusiwe kutoka nje ili kuweza kupata madini hayo kutoka kwenye udongo.

- Kuwapa vidonge vya madini ya chuma.

- UtoajiwaMeno

Siku chache baada ya kuzaliwa; meno kama sindano huchomoza katika taya zote mbili; Meno haya humumiza na kusababisha vidonda kwenye chuchu za mama wakati wanaponyonya. Hali hii humfanya mama kuwanyima watoto maziwa na kuwapiga, hivyo husababisha vifo vya watoto. Vile vile wao kwa wao huumizana.

Meno haya yafaa yakatwe kwa mkasi mkali na msafi. Kama yasipokatwa huweza kumuumiza hata mhudumiaji.

- Kukata Mkia

Mkia wa nguruwe unaweza kukatwa mara tu baada ya kuzaliwa ili wenyewe kwa wenyewe wasichezeane na kutafunana. Dawa ya lodine 5% ipakwe penye kidonda mara tu baadaya kukata mkia.

- Kulisha Chakula cha Kwanza.

Watoto wapewe chakula maalum kidogo kidogo kuanzia siku ya kumi baada ya kuzaliwa. Chakula hiki kinatakiwa kiwe na viinilishe vya kujenga mwili, kuleta nguvu na kuzuia maradhi. Wakiwa na umri wa wiki tatu wapewe gramu 450; wiki ya nne na ya tano wapewe gramu 680 kwa nguruwe kwa siku. Endelea kuwapa chakula hiki mpaka siku ya kuachishwa kunyonya, na vile vile wapewe maji kwa wingi.

- Kuhasi

Watoto madume ambao hawahitajiki kwa ajili ya kuzalisha wahasiwe wakiwa na umri kati ya wiki tatu hadi sita.

Nguruwe waliohasiwa huwa wapole, hunenepa haraka, huwa na nguvu na wazito kwa hiyo wanafaa kwa nyama na mafuta. Muone mtaalam wa mifugo kwa ajili ya kuhasi nguruwe wako

- Vitambulisho

Ngumwe hupewa vitambulisho kabla ya kuwatenganisha na mama yao kwa kuwaweka nambari kwenye masikio. Unashauriwa kumuona mtaalam wa mifugo akupe ushauri wajinsi ya kuweka vitambulisho hivyo.

- Kutenganisha Watoto na Mama Yao.

Watoto wakifikia wiki nane watenganishe na mama yao. Mama ahamishwe kwenye chumba na kuwaacha watoto ili kupunguza mgutusho wa kuhamia mahali pengine. Unapowatenganisha hakikisha unawapa dawa ya minyoo, unawakinga dhidi ya magonjwa na kuwatibu mara wanapougua.

Kukuza Nguruwe

- Walioachishwa Kunyonya

Nguruwe walioachishwa kunyonya wapewe chakula cha kukuzia. Badilisha chakula kwa utaratibu maalum kwani kubadilisha chakula ghafla kutoka cha watoto kuingia cha kukuzia kunaweza kusababisha matatizo ya tumbo. Changanya chakula cha watoto na cha kukuzia katika uwiano ufuatao: -

Wiki	Chakula cha Watoto	Chakula cha Kukuzia
1	Sehemu 3	Sehemu 1
2	Sehemu 2	Sehemu 2
3	Sehemu 1	Sehemu 3
4	Sehemu 0	Sehemu 4

Inashauriwa kuwapa chakula kama ifuatavyo:-

Wiki	Kiasi kwa Siku (kilo)
8 - 12	1.0
12 - 18	1.5
18 - 23	2.0
23 - 30	3.0

Lisha marambili kwa siku. Piawapewe maji safi yakutoshawakati wote.

Usafi wa chumba, vifaa na mazingira ni muhimu kila siku. Pawe na vitu vya kuchezea kama vile minyororo au matairi ili kumpa mazoezi, kuondoa upweke na kupunguza kupigana.

Endapo mkulima atahitaji nguruwe kwa ajili ya kuzalisha, wakati mzuri wa kuchagua ni wanapofikia umri wa miezi mitatu na kuendelea.

Nguruwe wanaweza kuchinjwa kwa ajili ya nyama wakiwa wamefikia uzito wa kilo 60 hadi 90. Ikiwa watakuwa wametunzwa vizuri watafikia uzito huo wakiwa na umri wa miezi 6 hadi 8.

SURA YA NNE

CHAKULA CHA NGURUWE

Nguruwe huhitaji kulishwa vizuri ili waweze kukua haraka na kufikia uzito wa kuchinjwa mapema.

Ikiwa watatunzwa vizuri watafikia uzito wa kilo 60 hadi 90 wakiwa na umri wa miezi sita hadi tisa.

Nguruwe ana uwezo wa kula vyakula vya aina mbali mbali ikiwa ni pamoja na mabaki ya vyakula vya nyumbani, shambani na viwandani.

Pamoja na vyakula hivyo, ni muhimu kumlisha chakula cha kutosha, bora na chenye viinilishe vyote vinavyohitajika mwilini. Hata hivyo ili kupunguza gharama mkulima anashauriwa kumlisha vyakula vinavyopatikana katika mazingira yake.

Mfugaji anaweza kuchanganya chakula mwenyewe au kununua kutoka kwenye maduka yanayouza vyakula vya mifugo. Mchanganyiko huo uwe na makundi mbali mbali ya vyakula.

Kuchanganya Vyakula

Chakula kamili lazima kiwe na makundi yote matatu ya kujenga mwili, kutia nguvu najoto na kulinda mwili.Vyakulavya kuchanganya vitatofautiana kutegemea na mahali au upatikanaji wa vyakula hivyo.

Mchanganyiko wa vyakula hivi uwe katika uwiano kufuatana na makundi mbali mbali kwa mfano, chakula cha kukuzia kiwe na:

	Asilimia
• Vyakula vya kutia nguvu najoto	65 hadi 75
• Vyakula vya kujenga mwili	20 hadi 25
• Vyakula vya kulinda mwili	
- Kalsiumu na Fosforasi	2 hadi 3
- Madini mchanganyiko na chumvi	1.5 hadi 2

Kiasi cha Viinilishe Muhimu Vinavyohitajika kwa Makundi Mbali mbali ya Nguruwe.

Viinilishe vya	**Nguruwe wadogo**	**Nguruwe wanaokua**	**Majike yenye mimba na kunyonyesha**	**Madume**
• kutia nguvu ajoto (Energy)	13	12.5	12.5	12.5

• Kujenga mwili (CP%)	20	16	14.5	14
• Kalsium (%)	0.90	0.75	0.75	0.55
• Fosforasi (%)	0.70	0.55	0.55	0.45

- Mfano wa chakula cha kukuzia Kilo 100

Aina	**Kilo**
Pumba za mahindi	45
Mahindi yaliyosagwa	30
Mashudu ya pamba/Alizeti	15
Dagaa	3
Damu iliyokaushwa	5
Madini	2
	100

SURA YA TANO

BANDA BORA LA NGURUWE

Ngumwe hawana uwezo mkubwa sana wa kustahimili hali ya baridi aujoto kwani hawana manyoya ya kuwasaidia kujikinga na baridi wala njia za kutoajoto. Kwa hiyo banda bora na malazi mazuri ni muhimu sana kwawanyama hawa. Ujenzi wabanda bora uzingatie mambo yafuatayo:

Uchaguzi wa Eneo Linalofaa

Eneo linalofaa kwa kujenga banda la nguruwe linatakiwa liwe nasifazifuatazo:-

- Eneo lisilotuamishamaji
- Lisiwe karibu na eneo wanaloishi watu
- Liwe mbali na chanzo cha maji kwa matumizi ya binadamu
- Liwe na sehemu ya kutupia kinyesi na uchafu mwingine kutoka bandani
- Liwe kubwa kuruhusu upanuzi wa baadaye
- Pawe rahisi kufikika kurahisisha usaflrishaji.

Sifa za Banda Bora

- Urefu wa banda ujengwe kuelekea kusini - kaskazini ili kupunguza kupenyeza kwa mionzi ya jua.

- Liwe kubwa kulingana na mahitaji

- Kuta ziwe imara, zilizojengwa kwa kutumia matofali ya saruji, mbao, mabanzi au boriti.

- Liwe na madirisha makubwa yanayoingiza hewa na mwanga wa kutosha.

- Sehemu za joto, nusu ya ukuta, sehemu ya chini ijengwe kwa matofali na sehemu yajuu ijengwe kwa wavu imara.

- Liwe na uzio kwa ajili ya mazoezi. Sakafu ijengwe kwa zege naiwena mteremko kurahisisha shughuli za usafi.

- Paa liwe imara lisilovuja. Linaweza kuezekwa kwa mabati, nyasi au makuti.

Sehemu za Banda

Banda la nguruwe ligawanywe katika sehemu mbali mbali kulingana na makundi yanayofugwa. Vile vile kuwe na sehemu ya stoo na ya kuchanganyia chakula.

Halikadhalika banda liwe na nafasi ya kutosha kwa kuhifadhi vyakula na vifaa vinavyotumika kuhudumia wanyama. Sehemu hizi daima ziwe kavu na zisizovuja.

Vipimo

Vipimo kwa ajili ya nafasi inayohitajika kwa makundi mbali mbali ya Nguruwe

Kundi	**Ukubwa wa Eneo kwa nguruwe (*Vipimo katika mita nwaba*)**
Dume	9
Jike:	
Sehemu ya kulala	1.28
Sehemu ya mazoezi	3 hadi 4
Chumba cha kuzalia pamoja na kreti	6.2
Sehemu ya kunyonyeshea pamoja na sehemu ya watoto.	10
Chumba cha wasionyonyesha:	
Sehemu ya kulala	0.4
Sehemu ya mazoezi	0.9
Nguruwe wanaokua (kilo 50 hadi 60)	0.73
Nguruwe wenye uzito zaidi ya kilo 90	0.93
Sehemu ya chakula kwa: nguruwe wa kunenepesha	0.2 hadi 0.3
Jike	0.35



Mchoro wa chumbu cha Dume



Mchoro wa chumba kwa ajili ya kukuzia nguruwe 8 hadi 10



Mchoro wa nyumba kwa ajili ya jike wanne



Chumba cha kunyonyeshea



Mchoro wa Chumba chu kunyonyeshea

SURA YA SITA

MAGONJWA NA MATATIZO YA NGURUWE

Magonjwa

Mfugaji anatakiwa kuzingatia afya ya mnyama ili pato liweze kuwa la kuridhisha. Hapa Tanzania magonjwa yanayosumbua nguruwe sio mengi lakini hutokea mara kwa mara kufuatana na umri, mazingira na afya ya mnyama.

Magonjwa huleta hasara kwa mfugaji kwani huweza kusababisha vifo, kupunguza uzito, ukosefu wa damu hasa kwa watoto na nguruwe kudumaa. Kwa hiyo ni vizuri kuyazuia na kutoa taarifa kwa mtaalam wa mifugo mara uonapo afya ya mnyama inabadilika.

Yafuatayo ni baadhi ya magonjwa yanayoshambulia nguruwe hapa nchini.

Ugonjwa	Husababishwa na	Dalili za Ugonjwa	Kinga na Tiba
Homa ya Nguruwe (African Swine Fever)	**Virusi** Huenezwa na Virusi • Nguruwe wagonjwa kuchanganyika na wasio wagonjwa • Kula chakula chenye virusi • Kupe laini	• Homa kali (41°C) • Kuhema sana • Kushindwa kala na kutembea • Rangi ya ngozi hugeuka kuwa bluu au nyekundu • Kifo baada ya siku 7. • Kuharisha • Huenea kwa kasi baada ya kutokea.	• Hakuna Tiba wala chanjo • Nunua nguruwe kwenye mashamba yasiyo na historia ya ugonjwa • Usafi wa vifaa, banda na mazingira yake • Nunua vyakula vilivyothibitishwa • Usitumie masalia toka sehemu zenye ogonjwa • Tumia dawa za kuua kupe. • Nguruwe wagonjwa wachinjwe.
Ugonjwa wa Ngozi	• Ukosefu wa vitamini • Huenezwa na Viroboto, Chawa, Inzi na Utitiri	• Kujikuna mara kwa mara. • Uvimbe kwenye ngozi. • Hushindwa kula vizuri • Hupungua uzito	• Ogesha nguruwe vizuri. • Tumia dawa ya kuua viroboto, chawa, Inzi na utitiri • Lisha nguruwe chakula chenye vitamini na madini ya kutosha.
Kichomi (Pneumonia)	Bakteria	• Homakali • Kupumua harakaharaka na kwa	• Hakuna tiba • Kiua bakteria hutumika kuzuia

		nguvu • Kikohozi kikavu	nmyama kushambuliwa na magonjwa mengine. • Kuwatenga wanyama. • Nyumba iwe na hewa na joto la kutosha.
Midomo na Miguu	Virusi • Huenea kwa kugusana mnyama mgonjwa na mzima au kula chakula chenye virusi	• Huwa na malengelenge miguuni, kwenye kiwele, midomoni na kooni. • Hushindwa kula na kutembea.	• Hakuna tiba • Apewe ohanjo • Asipewe chakula chenye virusi • Tibu Vidonda • Karantini ya sehemu yenye ugonjwa.
Kimeta (Anthrax)	Bakteria	• Uvimbe kwenye mgongo • Kupumua kwa tabu. • Kifo cha ghafla • Damu isiyoganda hutoka katika sehemu zilizo wazi kama mdomoni, masikioni na puani.	• Apewe chanjo • Nguruwe mgonjwa asichinjwe na aliyekufa asipasuliwe • Mzoga uzikwe katika kina cha zaidi ya mita mbili au kuchomwa moto • Toa taarifa kwa mtaalam wa mifugo haraka
Mafua (Swine influenza)	Virusi • Huenea kwa haraka kutokani na mabadiliko ya hali ya hewa	• Hudumaa • Hukohoa • Homa kali • Hamu ya kula hupungua. • Hupumua kwa taabu • Manyoya husimama bila mpangilio.	• Hakuna tiba wala chanjo • Banda liwe bora ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. • Zingatia kanuni za ufugaji bora.
Ugonjwa wa kuharisha hasa kwa nguruwe wachanga (Coccidiosis)	Bakteria • Huenea kwa mnyama kula chakula chenye bakteria hao. • Uchafu wa vifaa nabanda	• Huharisha mharo wa kijivu uliochanganyika na kijani • Hupungua uzito na kuwa dhaifu	• Usafi wavyombo na banda • Wape dawa aina ya Koksidiostant
Ugonjwa wa Ndorobo (Trypanosomiasis)	Protozoa • Huenezwa na mbung’o	• Hupungua damu • Hukonda • Manyoya yanasimama • Huweza kufa ghafla bila dalili za ugonjwa kujitokeza.	• Tumia madawa ya kuua mbung’o • Mazingira yawe safi wakati wote.

Matatizo

Ngumwe anaweza kukabiliwa na matatizo kama ya kutupa mimba, vifo, mshipa na kupata minyoo ikiwa hatatunzwa vizuri.

õ **Kutupa Mimba**

Ni tatizo linaloweza kutokea kama ngumwe atapata matunzo mabaya kama vile lishe duni, mgutusho au magonjwa. Kwa hiyo ngumwe atunzwe vizuri ili kuzuia magonjwa, mgutusho na asisumbuliwe wakati akiwa na mimba.

õ **Vifo vya Watoto**

Vifo vya watoto huletwa na baridi, kulaliwa na mama yao au udhaifu wa watoto wenyewe, kuhara, upungufu wa damu, ukosefu wa maziwa ya kwanza na kutouguza kitovu. Pia vifo hutokana na mama kushindwa kuzaa kutokana na nj ia ndogo ya uzazi au kupandishwa dume kabla maungo hayajakomaa vizuri. Mara nyingine vifo vya mama na watoto hutokea kama msaada haukutolewa upesi wakati nguruwe anapozaa. Ukosefu wa maziwa ya kutosha, pia huleta vifo kwa watoto.

Vile vile nguruwe waliotenganishwa na mama yao huweza kufa kama utaratibu wa kuwatenganisha haukufuatwa. Nguruwe watengwe kulingana na umri na uzito wao.

õ **Mshipa**

Mshipa ni tatizo la kurithi. Tatizo hili linapoonekana nguruwe dume achinjwe mara moja.

õ **Minyoo:**

Minyoo hutokana na uchafu wa mazingira ambao huathiri afya ya mnyama na hivyo hupunguza pato la mkulima.

Dalili za mnyama mwenye minyoo.

- Hukondeana na hukua taratibu
- Nguruwe wadogo hufa kutokana na minyoo kuziba utumbo mdogo.
- Hupungua damu
- Hupoteza hamu ya kula.

Kuzuia.

- Kuwapa dawa ya minyoo
- Kuzingatia usafi wa vyombo, banda, na mazingira yake.

õ **Kuumana kwa Nguruwe.**

Hii husababishwa na lishe duni ya wanyama na kukosekana kwa vitu vya kuchezea. Ili kuzuia hali hii, wanyama wapewe chakula bora na weka vitu vya kuchezea katika chumba.

SURA YA SABA

SOKO NA UTAYARISHAJI WA MAZAO

Ubora wa nyama na mafuta ya nguruwe unategemea kvva kiasi kikubwa utunzaji wa nguruwe ulivyokuwa. Hata hivyo baada ya kupata mazao hayo, ubora wake unaweza kuharibika kwa haraka sana na kusababisha hasara kwa mfugaji endapo taratibu za utayarishaji na hifadhi ya mazao hayo, hazitafuatwa. Ili kuzuia ubora usipotee na kuweza kupata soko zuri, ni muhimu matayarisho kabla ya kuuza yafanyike kwa makini.

Matayarisho ya Nguruwe Kabla ya Kuuza

Nguruwe wanaweza kuuzwa wakiwa hai au wakiwa wamechinjwa.

- Nguruwe kwa ajili ya kuchinjwa wakaguliwe na wasipewe dawa mwezi mmoja kabla ya kuchinjwa.

- Wasafirishwe kwa uangalifu wanapopelekwa kuchinjwa au kuuzwa.

- Kama watasafirishwa kwa gari basi liwe na nafasi za kupitisha hewa ya kutosha.

- Wasipewe chakula masaa 12 kabla ya kuwasafirisha.

- Wasisafirishwe wakati wajua kali, wamvvagiwe maji yabaridi kabla na wakati wa kuwasafirisha.

- Wawckewe matandiko, kuwe na kivuli na kusiwe nautelezi.

- Kuta za gari ziwe ndefu ili wasiweze kuruka.

- Usichanganye nguruwe wakubwa na wadugo wakati wa kusafirisha.

- Usisimame njiani wakati unapeleka nguruwe machinjioni.

Matayarisho Kabla ya Kuchinja

- Asipewe chakula masaa 12 kabla ya kuchinjwa.
- Apimwe na Bwana mifugo kabla ya kuchinjwa.
- Apimwe uzito kabla ya kuchinjwa.
- Sehemu ya kuchinjia iwe safi.
- Andaa vifaa vinavyohitajika kama, maji moto, visu, panga na shoka na viwe safi.

Utaratibu wa Kuchinja

• Nguruwe agongwe kichwani ili apoteze fahamu kidogo. Kisha mning’inize kwa kamba na mchinje kichwa kikiwa kimeelekea chini, kinga damu kwa ajili ya matumizi mengine.

• Mning’inize kwa muda kuhakikisha damu imetoka yote.

• Tumia maj i ya moto kuondoa manyoya kwa kukwangua na kisu.

• Pasua tumbo ili kutoa matumbo. Njia hii inasaidia kutochafua nyama kwa mabaki ya chakula tumboni.

• Nyama ikaguliwe na mtaalam wa mifugo kabla haijauzwa au kuhifadhiwa ili kuzuia kuenea kwa magonjwa.

Nyama inaweza kuuzwa nzima au ikiwa katika vipande vipande kufuatana na sehemu ya nyama. Ifungwe kwenye vifaa maalum na kuwekewa maelezo kama uzito, tarehe ya kuchinja na ya mwisho wa kutumia.

• Mafuta yatenganishwe na nyama.
• Nyama iwekwe kwenye chumba cha baridi.

Ukizingatia usafi na utaratibu mzuri wa kutayarisha mnyama utapatasoko zuri.

SURA YA NANE

KUWEKA NA KUTUNZA KUMBUKUMBU

Kuweka kumbukumbu ni jambo muhimu kwa kila shughuli inayotarajiwa kutoa mapato. Kumbukumbu katika maandishi zinasaidia kumuelewesha mfugaji hasara na faida zinazopatikana ambazo asingeweza kuzikumbuka kwa urahisi.

Shabaha nyingine za kuweka kumbukumbu ni kuweza kulinganisha maendeleo na ubora wa mifugo yako. Utaweza kuchagua nguruwe bora katika kundi, kufahamu ni yupi anayezaa watoto wengi na kuwatunza vizuri. Kumbukumbu itakufahamisha kiasi cha mapato uliyoyapata kutokana na aina fulani ya nguruwe na kulinganisha na nyingine kablahujaamua kuibadilisha.

Aina Za Kumbukumbu

- Idadi ya ngumwe wanaofugwa kwa ajili ya kuzaa, majike yaliyozaa madume na majike ambayo hayajazaa.

- Kiasi cha chakula kinachohitajika kwa kila ngumwe

- Uzito kila baada yajuma moja hasa kwa wale wanaofugwa kwa ajili ya nyama.

- Kumbukumbu za nguruwe mmoja, kwa mfano:

- Aina ya ngumwe
- Namba ya nguruwe
- Tarehe ya kuzaliwa
- Dume lililotumika
- Tarehe ya kuzaa
- Idadi ya waliozaliwa, wazima na waliokufa
- Uzito wa watoto walipozaliwa, baada ya wiki 3 na baada ya wiki 8.

Utunzaji wa kumbukumbu

Mifano ya kutunza kumbukumbu:-

Kadi ya Jike

Namba ya Jike ..... Tarehe ..... Aina .....

Namba ya baba ..... Namba ya mama .....

Tarehe ya kupandishwa	Namba ya dume	Tarehe ya kuzaa	Namba ya watoto	Idadi	Uzito wa	Tarehe ya kutenganishwa	Idadi ya waliotenganishwa

					juml a wazima/waf u			

Kadiya Dume

Namba ya dume ..... Tarehe ya kuzaliwa ..... Aina .....

Namba ya baba ..... Namba ya mama .....

Namba ya jike	Tarehe ya kupanda	Tarehe ya kuzaa	Wazima	Wafu	Jumla	Watoto waliotenganishwe		
						idadi	Uzito	Tarehe

Kadi ya kinga na matibabu

Tarehe	Namba ya nguruwe	Jinsia	Umri	Ugonjwa	Matibabu	Maelezo

Kumbukumbu ya maendeleo ya kundi zima

	Januari	Februari	Machi	Wastani baada ya miezi 6	Inavyotakiwa
Idadi ya majike					
Idadi ya watoto					
Idadi ya dume					
Waliopandwa hadi kuzaa					

Jike waliozaa
Watoto waliozaliwa hai
Asilimia ya waliokufa
Jumla waliozaliwa kwa jike moa
Waliozaliwa hai kwa jike moja
Vifo vya watoto
Vifo vya walioachishwa kunyonya
Vifo vya wanaonenepeshwa
Waliouzwa
Waliozaliwa jike moja kwa mwaka
Waliouzwa kutoka kwa jike moja kwa mwaka

ISBN 9987 647 01 4

Designed & Printed By: Ngulai Enterprises and General Supplies Printing Unit